



REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF ENVIRONMENT AND FORESTRY
KENYA METEOROLOGICAL DEPARTMENT
P.O BOX 30259-00100

NAIROBI

OCTOBER-DECEMBER, 2022 SEASONAL AGRO-WEATHER ADVISORY FOR KILIFI COUNTY



KENYA CEREAL ENHANCEMENT PROGRAMME-CLIMATE RESILIENT AGRICULTURAL LIVELIHOODS WINDOW (KCEP-CRAL)

Geoffrey Ogutu, CDMs Kilifi, Email: ogutugeoff@hotmail.com, WhatsApp: 0722890586

Getrude T.Leshamta CDMs Kilifi Email: gleshamta@gmail.com WhatsApp: 0720672579

Website: www.meteo.go.ke

KUHUSU MASHAURI HAYA

- ❖ Msimu wa mvua ya vuli unategemewa sana Kaunti ya Kilifi na haswa maenea yaliyo mbali na ufuo wa bahari.
- ❖ Ukulima hutegemewa na watu wengi kwa ajili ya lishe na kitega uchumi kwa njia ya ufugaji, ukulima nafaka, matunda na uvuvi.
- ❖ Mashauri haya yametokana na ushirikiano wa idara ya utabiri wa hali ya hewa, wataalamu wa kilimo na wakulima wa Kilifi.

KINA CHA MASHAURI

Mashaari haya yamependekezwa kuwamakinisha wakulima, wavuvi na washikadau wote kwa sekta mbalimbali ili:

- ❖ kufanya maamuzi ya busara ukiwemo mgao mbaya na mvua ya kiwango cha chini ya kawaida,
- ❖ kuwamakinisha wakulima kunufaika na vipindi vya mvua nzito,
- ❖ kuwamakinisha wakulima kujitahadhari na vipindi vya kiangazi,
- ❖ kuwapa mwongozo wa busara washikadau wote,
- ❖ kuhamasisha sekta zote za maamuzi ili kuendeleza kilimo kwa vizazi vijavyo kaunti ya Kilifi.

TAHADHARI

- ❖ Kiangazi cha Msimu huu wa mvua ya Vuli kimesababishwa na mfumo wa negative Indian Ocean Dipole (IOD) na LANINA.
- ❖ Mfumo wa Negative IOD huwa unasambaratisha mvua maeneo yetu. .
- ❖ Mfumo wa LANINA huwa unasambaratisha mvua maeneo yetu.
- ❖ Msimu wa mvua ya Vuli ukiwa unakutana na msimu wa Kaskazi huenda ukawa na michafuko ya bahari.
- ❖ Wavuvi wanaotumia maboti wanashauriwa kufuatilia jumbe zetu za hali ya hewa baharini tunazo wasilisha kupitia viongozi wa BMU na radio zote Kilifi kila juma.
- ❖ Inapendekezwa kua, utabiri huu wa msimu wa mvua ya vuli ufuatiliwe pamoja na ule wa kila juma ili kujimakinisha na mabadiliko yanayotarajiwa kusababishwa na mifumo mingineyo inayopatikana katikati ya msimu.

UTABIRI WA MVUA YA VULI, 2022

- ❖ Mvua ya vuli inatarajiwa kuwa kidogo na ya kiwango cha chini kupita kawaida.
- ❖ Mgao wa mvua utakua mbaya kwa wakati na sehemu.
- ❖ Vipindi vya kiangazi na mafuriko vinatarajiwa.
- ❖ Mvua itaanza kuchelewa(Tarehe 14-30 November).
- ❖ Mvua inatarajiwa kuisha mapema (Tarehe 19-31 December).
- ❖ Maeneo tofauti kurukwa na mvua inatarajiwa.
- ❖ Mda wa msimu unatarajiwa kua mfupi(siku 30-45)
- ❖ Kiwango cha mvua kinatarajiwa kuwa kati ya 139mm na 340mm chini ya kile cha kawaida 184mm hadi 427mm.
- ❖ Viwango vya joto vinatarajiwa kua vya juu zaidi hatimaye kuongeza makali ya ukame na kunawiri kwa viwavi.

N/B

- ❖ Kiwango cha chini cha mvua, mgao mbaya na kuchelewa kwa mvua ya vuli imetokana na kupoa kwa magharibi ya bahari ya Hindi ikipokelewa na hali ya LANINA maeneo ya equatorial Pacific.

OND 2022 AGRO-WEATHER ADVISORIES FOR KILIFI COUNTY

SUB-COUNTY	KIWANGO CHA MVUA KINACHOTARAJIWA KILA WARD	ZONI YA MVUA	SAMPULI YA MIMEA YA KUPANDWA
Ganze	Bamba: 190-290mm Ganze:240-290mm Jaribuni: 190-290mm Sokoke: 240-290mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA CHINI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Nyasi Miti inayostahimili ukame Miche ya Melia

Kaloleni	Kayafungo: 240-340mm Mwanamwanga: 240-340mm Mariakani: 240-340mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA CHINI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties) Mahindi (DH02, PH1 ukitumia kilimo hifadhi)
	Kaloleni: 290-340mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA WASTANI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties) Mahindi (DH02, PH1 ukitumia kilimo hifadhi)
Kilifi South	Junju: 190-290mm Chasimba: 190-290mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA JUU	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties)
	Mtepeni: 240-290mm Mwarakaya: 240-290mm Shimo la Tewa: 240-290mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA JUU	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties) Mahindi (DH02, PH1 ukitumia kilimo hifadhi)
Kilifi North	Matsangoni:190-290mm Tezo: 190-240mm . Kibarani: 190-240mm . Sokoni: 190-240mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA JUU	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties)

	Dabaso: 190-240mm . Watamu: 190-240mm .	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA WASTANI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties)
	Mnarani: 190-240mm .	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA JUU	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties) Mahindi (DH02, PH1 ukitumia kilimo hifadhi)
Malindi	Kakuyuni: 190-240mm Shella: 139-240mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA WASTANI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties)
	Jilore: 190-290mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA CHINI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties)
	Ganda: 139-240mm Malindi:139-240mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA WASTANI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties) Mahindi (DH02, PH1 ukitumia kilimo hifadhi)
Magarini	Garashi: 190-290mm Adu: 190-290mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha

	Gongoni: 139-190mm Marafa: 190-290mm	CHA CHINI	Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties)
	Sabaki:139-190mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA WASTANI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties)
	Magarini:139-240	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA WASTANI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties) Mahindi (DH02, PH1 ukitumia kilimo hifadhi)
Rabai	Kambe Ribe: 290-340mm Mwawesa: 290-340mm Rabai: 290-340mm Ruruma: 290-340mm	ZONI YA MVUA YA KIWANGO CHA WASTANI	Mtama (Gadam variety) Kunde mboga/nafaka (M66, Kenkunde, K80 varieties) Mchicha Mawele Pojo/ndengu (KS20, N26 varieties) Mahindi (DH02, PH1 ukitumia kilimo hifadhi)

MASHAURI YA METEOROLOGICAL

- ❖ Wakulima wanashauriwa kushirikiana na afisaa wa kilimo nyanjani.
- ❖ Panda mimea inayostahimili ukame.
- ❖ Panda mimea inayokomaa haraka.
- ❖ Panda mara tu kutakavyonyesha siku tatu mfulilizo Zaidi ya 20mm au mchanga unapolowa vizuri ukifuatilia jumbe zetu za kaunti kila wiki.
- ❖ Tumia mbinu za kilimo hifadhi ili kujinufaisha na vipindi vya mvua nzito na kustahimili vipindi vya kiangazi.

- ❖ Wakulima wanahamasishwa kujihami dhidi ya uwezekano wa kuongezeka kwa viwavi kwa ajili ya viwango vya juu vya joto.
- ❖ Wanaoishi maeneo ya mafuriko wanashauriwa kuchukua tahadhari za matukio ya mvua nzito ukiwemo ukame.
- ❖ Barabara mbovu zitahitajika kukarabatiwa ili kudhibiti matukio ya mvua nzito.
- ❖ Kwa ajili ya ukame, shule zitahitaji msaada wa chakula, maji na karo haswa maeneo kame ya Kilifi yaliyorukwa na mvua kwa Zaidi ya misimu minne mtawalia.
- ❖ Msimu wa vuli ukiwa pia ni msimu wa Kaskazi unahitaji kuchukuliwa kwa makini baharini na wavuvi wanaotumia madau na maboti madogomadogo.
- ❖ Pata jumbe zetu kupitia Radio SBS FM, PWANI FM, MTSENANGU FM, RADIO KAYA, LULU FM, KMA, KMD website.

Tumia Jumbe hizi pamoja na zile za kila juma/mwezi kutoka kwa county Director.

Kenya Meteorological Department imepewa jukumu la kutoa huduma za utabiri wa hali ya hewa ili kuhifadhi masingira, kulinda mali na usalama kutokana na athara za hali ya hewa.